**JUMUIYA YA MAENDELEO MBEZI BEACH 'A'**
S.L.P 3521,
DAR ES SALAAM
info@mbezibeach.or.tz
www.mbezibeach.or.tz
**+255 752 181 988**

**07 March 2026**

# RISALA FUPI YA KUMKARIBISHA MHESHIMIWA MKUU WA WILAYA YA KINONDONI NA KUOMBA USHIRIKIANO WA USIMAMIZI WA TAKA – MBEZI BEACH 'A'

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Mhe. Saad Mtambule, Viongozi wa Manispaa ya Kinondoni, viongozi wa Kata ya Kawe, viongozi wa Serikali ya Mtaa Mbezi Beach 'A', wageni wetu kutoka taasisi na asasi zisizo za kiserikali na vikundi mbalimbali vya usafi wa fukwe, wageni waalikwa, wana-JMMBA, na wakazi wenzangu wa Mbezi Beach 'A', habari za leo.

Awali ya yote tunamshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujalia uhai na afya, na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya zoezi hili la pamoja la usafi na utunzaji wa mazingira yetu.

Kwa utambulisho, Jumuiya ya Maendeleo Mbezi Beach 'A' (JMMBA) ni jumuiya ya wakazi wa eneo hili iliyoanzishwa kuunganisha nguvu za wananchi katika masuala ya maendeleo ya mtaa, hususan mazingira, miundombinu, ulinzi na usalama, na ushirikiano na Serikali ya Mtaa katika kutatua kero za wananchi. Jumuiya hii ilisajiliwa rasmi tarehe 13 Aprili 2024 chini ya Mrajisi wa taasisi zisizo za kiserikali, Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa mujibu wa Sheria ya Jumuiya Sura ya 337 (***Societies Act [Cap 337 R.E. 2002],*** ikiwa na namba ya usajili **S.A.23934**.

.

Kwa niaba ya JMMBA na kwa kushirikiana na Ofisi ya Serikali ya Mtaa Mbezi Beach 'A', tunakukaribisha kwa heshima na taadhima katika ufukwe wetu. Ujio wako leo unaipa nguvu, kazi ya wananchi na unaonesha kwamba Serikali na jamii tunaweza kushirikiana kubadili mazingira kwa vitendo. Kaulimbiu yetu ni: ***Ufukwe Wetu, Wajibu Wetu, Tumerithishwa, Tuwarithishe.***

Mbali na usafi wa ufukwe, kama JMMBA kupitia kamati yetu ya Mazingira tunalipa kipaumbele pia suala la uboreshaji wa mazingira kwa ujumla. Tayari tumeanzisha mpango wa upandaji miti ambapo kila nyumba inahimizwa kupanda angalau miti miwili. Kwa faraja, baadhi ya wakazi na wanachama wetu wameshaanza kupanda miti, ikiwemo miche ya midodoma, na tayari eneo linaanza kupendeza. Tunatarajia kuendelea kuhamasishana na kusimamia mpango huu ili Mbezi Beach 'A' iwe kijani, safi na yenye kuvutia zaidi kwa makazi na kwa vizazi vijavyo.

**Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya**, Tangu tarehe 7 Februari 2026 tumekuwa tukifanya usafi wa ufukwe huu kila Jumamosi mfululizo bila kukosa. Kwa wiki nne tumekusanya mifuko 217, 304, 291 na 88, jumla mifuko 900, ndani ya takribani mita 200 tulizoweza kuzifanyia usafi kwenye awamu hii ya kwanza kati ya takriban mita mia tisa (900) za ufukwe huu wa Mbezi Beach A.

Huu ni ushahidi kwamba jamii tayari imeanza kufanya kazi, hususan kwenye **plastiki na taka ngumu** zinazoonekana kuongezeka kila wiki.

**Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya,** Hatua muhimu tuliyoanza tangu tarehe 28 Februari ni kuhamia kwenye usafi unaoendeshwa kwa takwimu, si hisia pekee. Ndiyo maana, kwa msaada wa wataalam wa washirika wetu wa usafi wa fukwe, tumeanza kutumia *WABA Methodology (Waste Assessment and Brand Audit).* Huu ni mfumo wa kitaalamu unaotusaidia kuhesabu taka tunazokusanya, kupima uzito, na kurekodi taarifa kwa muundo unaoweza kulinganishwa zoezi hadi zoezi. Faida yake ni kwamba tunapata takwimu zinazotuwezesha kupanga vizuri mahitaji ya vifaa na nguvu kazi, na pia kutoa ushahidi unaoaminika kwa wadau wa kitaifa.

Katika zoezi la tarehe 28 Februari 2026, tulipima kwa utaratibu na kupata wastani wa uzito wa kilo 11.61 kwa mfuko, tuseme kilo 12. Kwa kipimo hicho, mifuko 900 tuliyokusanya ndani ya wiki nne inawakilisha takribani tani 10 hadi 11 za taka ngumu tulizoondoa kwenye ufukwe ndani ya takribani mita 200 tulizoweza kuzifanyia usafi kwenye awamu hii ya kwanza kati ya mia tisa za ufukwe wetu huu wa Mbezi Beach A (Rainbow). Takwimu hizi zinakusudiwa pia kuingizwa kwenye mifumo ya kitaifa kama ***National Plastic Action Partnership (NPAP***) ili kazi ya wananchi iwe na ushahidi wa kitaalamu na kusaidia upangaji wa hatua dhidi ya uchafu wa plastiki.

**Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya,** changamoto yetu kubwa baada ya kukusanya taka ni uondoaji wake. Kwa maelezo tuliyopata, mkandarasi wa taka za majumbani anafanya kazi chini ya utaratibu unaolipiwa kupitia makusanyo ya kaya, hivyo taka za ufukwe kama hizi haziingii moja kwa moja kwenye huduma hiyo bila mwongozo maalum wa Manispaa. Tumeelezwa pia kuwa huduma kama hii inapohitajika hutazamwa kama safari maalum yenye gharama ya ziada, Kwa mantiki hiyo, tunaomba Manispaa iweke utaratibu rasmi, ikiwemo afisa anayehusika moja kwa moja na jambo hili, ili jamii

inapokuwa na mazoezi ya usafi wa kijamii kama hili pawepo njia ya haraka, ya wazi na ya moja kwa moja ya kuratibu uondoaji wa taka zilizokusanywa.

Mpango wetu siyo kufanya usafi kwenye eneo hili la ufukwe wa bahari tu, bali ni kuona Mbezi Beach A yote inakuwa safi, kuanzia mitaani, kwenye maeneo ya wazi, mpaka ufukweni.

Pamoja na plastiki na taka ngumu, ufukwe wetu pia hupokea taka nyingi za asili zinazooza kama mwani, magogo ya miti, majani ya baharini, maganda ya nazi na majani ya minazi. Kwa uangalizi wetu wa eneo, zinaonekana kuwa na uzito mkubwa zaidi, na hatua inayofuata ni kuanza kupima rasmi ili tuwe na takwimu kamili na mpango wa kuziondoa kwa njia ya kuchakata, badala ya kuzihamisha tu kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

**Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya**, pamoja na uondoaji wa taka tulizokusanya, kuna chanzo kimoja kikubwa kinachoendelea kurejesha uchafu ufukweni kila wiki. Kwa uzoefu wetu wa kuja kila mwisho wa wiki, tumebaini kuwa kuna mto/korongo ambao, kutokana na ujenzi holela na sababu nyingine za kimazingira, umeacha njia yake ya kawaida na sasa unaelekeza maji na taka moja kwa moja kwenye ufukwe wetu badala ya kuingia baharini kwa njia iliyo sahihi. Kila mvua inaponyesha, taka ngumu kutoka juu huteremka na kusambaa ufukwe mzima, na hivyo kazi yetu ya wiki inaonekana kuanza upya.

Kwa heshima na taadhima, tunaomba tathmini ya kiufundi ifanyike haraka, kupitia Manispaa na mkandarasi husika, ili kuangalia namna bora ya kurekebisha mwelekeo wa mtiririko huo na kuurudisha uelekee baharini kwa usalama. Sambamba na hilo, tunaomba kuzingatiwa uwekaji wa kifaa cha kudhibiti uchafu kama wavu/kinga ya taka kwenye mdomo wa mto, ambacho kitapitisha maji lakini kitazuia na kukusanya taka ngumu. Hatua hii itasaidia

taka nyingi kukamatwa kwenye sehemu moja, na itafanya iwe rahisi kuzichambua na kuziondoa kila wiki bila kusambaa kwenye ufukwe mzima.

**Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya**, Kwa heshima na taadhima, tunapenda kutumia ujio wako leo kama fursa ya kuimarisha ushirikiano wa jamii na Serikali katika usimamizi wa taka, hususan plastiki na taka ngumu, na pia takaozo pale inapohitajika. Tumeuona na kuupokea mwito wa Serikali uliotolewa hivi karibuni na **Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Dkt. Festo Dugange**, kuhusu kukusanya takaozo na kuzipeleka kwenye uchakataji ili zitumike kama malighafi ya mboji, pamoja na kuandaa mkakati wa kuwahamasisha wananchi waone taka ni fursa. Kwa msingi huo, na kwa kuzingatia jitihada ambazo jamii tayari imeanza, Mbezi Beach ‘A’ iko tayari kuwa eneo la majaribio ndani ya Wilaya ya Kinondoni, na tunaomba uongozi wa Wilaya utambue na uidhinishe mpango huu kama pilot ya Wilaya ya Kinondoni, ili utaratibu wa ukusanyaji, uondoshaji na kupeleka takaozo kwenye uchakataji uanze hapa, kisha uongezwe hatua kwa hatua kwenye maeneo mengine ya wilaya.

**Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya,** tunaomba support yako katika mambo makuu yafuatayo:

**Kwanza,** tunaomba tathmini ya kiufundi ifanyike haraka kupitia Manispaa na mkandarasi husika kuhusu mto/korongo unaoleta taka ufukweni kila mvua inaponyesha, ili urejeshwe kwenye mwelekeo salama wa kuingia baharini na, pale inapofaa, kuwekwa wavu/kinga. (***litter trap / trash interceptors)*** – ambazo ni mfano wa mifumo inayotumika kwenye mito kuzuia taka za plastiki na taka ngumu kuingia baharini

**Sambamba na hilo,** tunaomba Wilaya na Manispaa ziimarishe usimamizi wa utupaji taka kwenye mto/korongo, ikiwemo kutoa maelekezo ya ufuatiliaji na udhibiti kwa viongozi wa ngazi ya mtaa/kata, kuzuia wananchi na biashara kutupa taka mtoni, na kuhakikisha taka zinaelekezwa kwenye mfumo rasmi wa ukusanyaji na dampo *(Kuacha kutumia mikokoteni)*.

**Pili,** tunaomba Afisa Maalum *(focal person)* mwenye mamlaka kutoka Manispaa au idara husika, awe kiungo cha mawasiliano na uratibu wa uondoaji wa taka za ufukwe na maeneo ya umma, pamoja na ufuatiliaji wa utekelezaji wa maelekezo haya.

**Tatu,** tunaomba maelekezo ya kuwekwa ratiba ya ukusanyaji *(pickup schedule)* ya uhakika ya kuchukua taka hizi na kuzisafirisha kwa utaratibu rasmi, ama kupitia mkandarasi au gari la Manispaa, ili tusibaki kwenye malipo ya dharura ya kila safari na ili kazi hii iwe endelevu.

**Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya,** Kwa upande wetu, tunaahidi kuendelea na usafi wa kila wiki, kuimarisha utenganishaji wa Plastiki, taka ngumu, pamoja na taka zinazooza, na kuboresha uandishi wa takwimu ili ushahidi wa kazi yetu uendane na uhalisia wa kazi inayofanyika ufukweni. Tukitekeleza hatua hizi kwa ushirikiano, matokeo yatakuwa ya wazi: ufukwe wetu utakuwa safi na salama kwa afya na matumizi ya wananchi, uchafu wa plastiki unaoingia baharini utapungua, na taka zinazooza zitapata mwelekeo wa kuchakatwa badala ya kubaki mzigo wa kudumu.

**Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya,** Zoezi hili linaunga mkono Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa *(United Nations Sustainable Development Goals – SDGs)*, hususan SDG 14 *(Life Below Water)* kwa kupunguza uchafu unaoingia baharini, SDG 11 *(Sustainable Cities and Communities)* kwa kuboresha usafi na matumizi salama ya coastline, SDG

12 *(Responsible Consumption and Production)* kupitia utenganishaji na usimamizi bora wa taka, SDG 3 *(Good Health and Well-being)* na SDG 6 *(Clean Water and Sanitation)* kwa kulinda afya, usalama na ubora wa maji, pamoja na SDG 17 *(Partnerships for the Goals)* kwa kuunganisha nguvu za jamii, Serikali ya Mtaa na wadau wengine.

**Karibu sana Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya**. Tunakushukuru sana kwa kufika, kwa kutusikiliza, na kwa kututia moyo juhudi za wananchi wa Mbezi Beach A. Karibu uone kazi ya wananchi wako. Karibu utupe maelekezo ya utekelezaji. Na karibu tushirikiane kuifanya Mbezi Beach ‘A’ iwe mfano wa Wilaya ya Kinondoni katika usafi wa fukwe na usimamizi wa taka. Tunakukaribisha pia siku nyingine uje uone maendeleo ya kazi tuliyoianza na matokeo yatakayopatikana kupitia ushirikiano huu.

**Asante sana kwa kunisikiliza.**

**Nakala kwa:**

1. **Mkurugenzi wa Manisapaa ya Kinondoni**
2. **Diwani Kata ya Kawe**
3. **Mtendaji Kata ya Kawe**
4. **Mwenyekiti Serikali ya Mtaa Mbezi Beach A**